**FOMU NAMBA………………………**

**ASSURANCE SECONDARY SCHOOL (DAY AND BOARDING SCHOOL, KATA YA MSONGOLA MTAA WA MVULENI. P.O.BOX -80865 DAR ES SALAAM TEL.0767414081/0767006553/0742500221/0768420412.**

**E-mail.assurancess2021@gmail.com. Reg .no.s5615 and centre NO. s6300.**

**MZAZI/MLEZI-----------------------------------------------------------------------------------**

**YAH: MALEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA 1,2,3 AU 4. KATIKA SHULE YA SEKONDARI ASSURANCE MWAKA ………………..**

**Ninayo furaha kukufamisha kuwa mtoto wako ………………………………………………….**

**Ni miongoni mwa wanafunzi wachache waliopata fursa ya kuendelea na masomo ya kidato cha 1,2,3,4. Katika shule ya sekondari Assurance, hongera sana kwa fursa hiyo. Kwa barua hii nakuletea fomu ya kujiunga na shule ya sekondari Assurance kwa mwanao.**

**Tafadhali nakuomba wewe na mwanao msome maelekezo haya kwa kina na kisha makamilishe yale yote yanayotokiwa. Pamoja na kuyasoma kwa kina naomba uendendelee kumshauri mwanao juu ya kutumia nafasi hii adimu aliyoipata vema ili lengo na azma yake itimie pamoja na lengo kuu la shule la ufaulu wa daraja la kwanza tu mwisho pointi 14 sawa na wastani wa 65. Nakutakia maandalizi mema na karibu sana Assurance sekondari.**

**WAMBURA DANIEL NYAMOHANGA**

**MKUU WA SHULE**

**FOMU NAMBA………………………**

**ASSURANCE SECONDARY SCHOOL (DAY AND BOARDING SCHOOL, KATA YA MSONGOLA MTAA WA MVULENI. P.O.BOX -80865 DAR ES SALAAM TEL.0767414081/0767006553/0742500221/0768420412. E-mail.assurancess2021@gmail.com. Reg .no.s5615 and centre NO. s6300.**

**FEES STRUCTURE /MGAWANYO WA ULIPAJI ADA KWA MWAKA 2023/2024.**

**FORM ONE, TWO AND THREE FEES PAYMENTS**

| S/N | ITEMS | FIRST INSTALLMENT JAN-MARCH | SECOND INSTALLMENT APRIL-JUNE | THIRD INSTALLMENT JULY-SEPTEMBER | TOTAL |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | TUTION FEES (ADA) | 1,800,000/- | | | 1,800,000/= |
| 2. | REMEDIAL AND EXAMS F2 ONLY | 220,000/= | | | 220,000/= |
| 3. | F1/3 | 700,000/- | 550,000/- | 550,000/- | 1,800,000/- |
| | F2 | 720,000/- | 650,000/- | 650,000/- | 2,020,000/- |

**FORM FOUR FEES PAYMENT**

| S/N | ITEMS | FIRST INSTALLMENT JAN-MARCH | SECOND INSTALLMENT APRIL-JUNE | THIRD INSTALLMENT JULLY – SEPTEMBER | TOTAL |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | TUTION FEES (ADA) | 1,800,000/= | | | 1,800,000/= |
| 2. | EXAMINATIONAND REMEDIALS | 230,000/= | | | 230,000/= |
| 3 | GRADUATIONS | 50,000/- | | | 50,000/- |
| | THREE INSTLAMENTS | 720,000/- | 680,000/- | 680,000/- | 2,080,000/- |
| DAY | F1/3 | 700,000/- | 350,000/- | 350,000/- | 1,200,000/- |
| | F2/4 | 700,000/- | 360,000/- | 360,000/- | 1,420,000/- |

**MALIPO YAFANYIKE KUPITIA AKAUNTI CRDB 0150248421200:**

**JINA LA AKAUNTI :ZAWADI NURSERY AND PRIMARY SCHOOL. GHARAMA ZA FOMU PAMOJA NA INTERVIEW -40,000/=**

**NOTE. SARE ZOTE ZA SHULE KAMA ZILIVYO UKURASA WA NNE GHRAMA YAKE NI 260,000/-**



**Fomu Namba……**

**ASSURANCE SECONDARY SCHOOL**
**P.O BOX – 80865 DAR ES SALAAM TEL. 0767414081/0767006553/**
**0742 500 221. WEBSITE: Zawadischools.ac.tz**

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ASSURANCE.**

**Ninayo furaha kukufamisha kuwa mwanao ……………………………………….. amechaguliwa kujiunga kidato cha 1, 2, 3, 4. Katika shule ya sekondari Assurance. Na anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……/…../………. Akiwa amekamilisha yale yote aliyoelekezwa katika fomu hii.**

1. **MAHALI SHULE ILIPO:**
   Shule ya Sekondari Assurance ipo Dar es salaam katika Wilaya ya Ilala kata ya Msongola, mtaa wa Mvuleni karibu na nyumba za wahanga wa mabomu ya Gongo la Mboto, kituo maalum cha bodaboda kwa Guragura. Kutoka mbezi stendi ya mkoa panda magari ya gongo la mboto shuka banana panda magari ya fremu kumi chukua pikipiki hadi shuleni. Kutoka kariakoo panda magari ya kivule sokoni shuka panda bajaji hadi msongola chukua pikipiki hadi shuleni. Senta kuu ya kuingia shuleni ni msongola magengeni.

2. **MAAGIZO NA MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE**
   **Ili mwanao apokelewe shuleni, anatakiwa afanye yafuatayo:**
   **Awasilishe hapa shuleni fomu ya vipimo iliyojazwa na daktari yeyote wa hospitali ya serikali baada ya kupimwa. Fomu hiyo iambatanishwe na barua hii. Afike na hati ya matokeo ya darasa la saba, prem number na jina la shule aliochaguliwa kwenda na nakala ya cheti cha kuzaliwa.**
3. **SARE ZA SHULE. ZOTE ZINAPATIKANA SHULENI. KWA TSH. 260,000/-**

**i.** **Suruali mbili nyeusi zenye malinda mawili wavulana, pindo [turn up] na zisizobana zenye upana wa si chini ya sentimiti 15 na soksi nyeusi [ asiyefuata maagizo haya hatapokelewa]. ,**

**ii.** **wasichana sketi ndefu kufuka magoti inchi nne au kutoka ardhini inchi nne malinda manne, soksi nyeupe.[asiyefuata maelekezo haya hatapokelewa]**

**iii.** **Shati mbili nyeupe mikono mifupi yenye nembo ya shule.**

iv. **Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili vya kufunga na kamba [lizingatiwe]**
v. **Sweta moja muundo wa v rangi ya buluu.**
vi. **T. shirt yenye kola marufu kama form six, rangi ya kijivu.**
vii. **Mkanda mweusi jozi usiwe na urembo wa kawaida.**
viii. **Kanda mbili jozi mbili. Ziwe za kawaida.**
ix. **Tai mbili ndefu za dark blue.**

**3**

**SARE ZA KUSHINDIA.**

I. **Suruali/sketi mbili za kitambaa rangi ya kijivu zenye mkunjo [turn up/in] zisizo za kubana, upana si chini ya sentimiti 17.**
II. **Track suti mbili rangi ya buluu.**
III. **Mshati mawili mikono mifupi ya light blue kwa ajili ya kuendea ibada.**
IV. **Viatu vya kushindia – raba za michezo nyeusi wavulana na wasichana nyeupe. Mfano jezi ya paris saint German. Vifaa kwa ajili ya michezo vitapatikana shuleni.**

**SARE ZA MICHEZO.**

I. **Raba /viatu rangi yoyote,**
II. **Bukta ,t-shirt na soksi ndefu vyote rangi ya dark blue.**

**NB: mwanafunzi hatarusiwa kuwa na mavazi mengine Zaidi tofauti ya haya yalioelekezwa.**
**Sare zote zitapatikana shuleni kwa shilingi 260,000/-**

**KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE:**

**KANUNI KUU NI KAULI MBIU YETU NA MOTTO WETU**

**MOTTO: STRIVING FOR EXCELLENCE.**

**KAULI MBIU YA SHULE. 'USE YOUR COMMON SENSE, DO WHAT BROUGHT IN ASSURANCE AND LET YOUR LIGHT SHINE'**

A) **MAHUDHURIO**
Mwanafunzi hana budi kuhudhuria vipindi vyote vya masomo darasani kwa siku zote za masomo kwa mwaka, asilimia mia moja, ruhusa kwa ugonjwa au kifo tu, vinginevyo sababu maalum. Ruhusa ya kwenda nyumbani itatolewa na mkuu wa shule tu.

B) **SHERIA ZA SHULE**
I) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule muda wote awapo shuleni ipasavyo hii ni pamoja nakuchomekea shati na kufunga mkanda vizuri.
II) Shati la shule ni lazima liwe na nembo ya shule

III) Nywele ziwe fupi mkato wa kawaida bila mtindo wowote,bwenzi, kipara, kiduku haviruhusiwi

IV) Mwanafunzi hana budi kuwatii na kuwaheshimu watu wa rika zote ndani na nje ya shule

V) Ni marufuku kwa wanafunzi kuvaa aina yoyote ya urembo ikiwa ni pamoja na pete, bangili, mikufu n.k

VI) Epuka vitendo viovu kama matusi, utoro, wizi, ugomvi, bangi, uasherati, ushoga, kuoa au kuolewa, kuchochea migomo n.k

VII) Ni lazima kwa wanafunzi kuwepo mahali sahihi kwa wakati sahihi ikiwa ni pamoja na kuhudhuria kwenye VIPINDI VYA DINI kulingana na ratiba ya shule inavyoelekeza

VIII) Timiza wajibu wako na kazi uliyopangiwa kwa wakati

IX) Mwanafunzi haruhusiwi kuandika mahali popote pasipo husika kama vile kwenye kuta, kwenye vitabu, kwenye samani za shule n.k

X) Hairusiwi kupiga au kupigana nje na ndani ya shule

C) **<u>HATUA ZICHUKULIWAZO KWA KUKIUKA TARATIBU NA SHERIA ZA SHULE</u>**

I. Kuonywa
II. Kufanya kazi za mikono zaidi
III. Kuchapwa viboko
IV. Kusimamishwa shule

D) **<u>MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA</u>**

a) Wizi
b) Uasherati
c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
d) Uvutaji bangi
e) Makosa ya jinai
f) Kupiga na kupigana
g) Kuoa au kuolewa na ushoga
h) Kudharau bendera ya taifa
i) Kupata, kutoa au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
j) Kugoma, kuchochea au kuanzisha vurugu au migomo
k) Kugomea adhabu kwa makusudi
l) Kukutwa na simu, line ya simu na vifaa vyovyote vinavyohusiana na simu
m) Kushiriki vitendo vya ugaidi
n) Kukaa nje ya shule kwa muda mrefu bila taarifa yoyote
o) Kutofanya mtihani bila sababu maalumu
p) Kushindwa kufikisha wastani wa 65 kwa kila somo au jumla ya masomo yote.

E) **<u>SHERIA ZA BWENINI</u>**

I) Kila mwanafunzi lazima azingatie usafi wa ndani na nje ya bweni
II) Ni marufuku mwanafunzi kuacha kitanda chake bila kutandika
III) Hairuhusiwi kuanika au kutundika nguo ndani ya bweni
IV) Ni marufuku kuingiza silaha ya aina yoyote kama vile rungu, kisu, nyundo, panga
V) Muda wa kulala ni kuanzia saa nne kamili usiku
VI) Hairuhisiwi kukosekana katika kitanda chako wakati wa kulala
VII) Ni marufuku kuchora, kuandika au kukwaruza kuta ndani na nje ya bweni
VIII) Hairuhusiwi kukaa bwenini wakati wa masomo au muda mwingine usiotakiwa bila ya idhini ya mwalimu wa bweni
IX) Hairuhusiwi kuingia au kula chakula bwenini

F) **<u>MAHITAJI MENGINE MUHIMU (MWANAFUNZI AJE NAYO SIKU YA KURIPOTI SHULE)</u>**

a) Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kisigino kifupi, visivyochongoka viwe vyenye kamba na siyo raba
b) Mkanda mweusi wa ngozi wenye chuma cha kawaida (kwa wavulana)
c) Madaftari makubwa 11 (counter books quire three)
d) Mathematical set moja kubwa
e) Kalamu za wino na penseli za kutosha
f) Rim paper moja (A4 size)
g) Vitabu kwa ajili ya kujisomea masomo yote
h) Begi la kubebea vifaa vya darasani
i) Godoro moja mbili na nusu kwa sita nchi nne.
j) Vindoo viwili vya kuogea na kufulia nguo, lita kumi.
k) Sahani moja yenye patisheni, kikombe nusu lita, kijiko, uma na chupa ya maji ya kunywa moja.
l) Kanda mbili pea moja,
m) Mashuka ya pink kwa wasichana, na buluu kwa wavulana.

G) **<u>MAHITAJI MUHIMU KWA WANAFUNZI WA BWENI</u>**

a) Taulo na sanduku lenye kufuri la kuhifadhi vitu vyako mfano nguo n.k
b) Raba za michezo

**<u>VIFAA VYA USAFI WA MAZINGIRA.</u>**

**I. Soft bloom moja**
**II. Squizer moja**
**III. Hard broom moja.**
**IV. Mfagio wa chelewa mmoja**
**V. Kwanja moja**
**VI. Jembe moja lenye mpini imara.**

H) **<u>VIFAA VYA USAFI BINAFSI.</u>**

a) Vifaa vingine muhimu mfano, sabuni za kuogea, kufulia za kutosha, mswaki na dawa ya meno.

**“Angalizo”** Ni marafuku kwa mwanafunzi kuja na vitu vya thamani kama vile redio, TV, laptop, simu



ASSURANCE SECONDARY SCHOOL, P.O. BOX 80865, DAR ES SALAAM.

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

TO
THE MEDICAL OFFICER
………………………………...
…………………………………
…………………………………

Please examine……………………………………as to his/her fitness for pursuing further education at our school

1. Haemoglobin ………………………………………………………………………
2. P.V bleeding……………………………………………………………….………..
3. a) Sight ……………………………………………………………………………..
   b) Hearing……………………………………………………………………………..
4. Blood pressure…………………………………………………………….………
5. Urine for sugar and pregnancy test(females)……………………………………
   ……………………………………………………………………………….………..
6. Stool for routine examination ……………………………………………………
7. Asthma…………………………………………………………………………………
8. Skin diseases……………………………………………………………………….
9. Leprosy…………………………………………………………………………………
10. Epilepsy……………………………………………………………………………….
11. Pulmonary tuberculosis…………………………………………………………
12. Deformity……………………………………………………………………………..
13. Mental problem……………………………………………………………………
14. Diabetes mellitus…………………………………………………………………
15. Hypoglycemia……………………………………………………………………...
16. Blood for widal test………………………………………………………………
17. Major operation (s)……………………………………………………………..…
18. Peptic ulcers (P.U)……………………………………………………….………..
19. Scrotal pain and swelling……………………………………………………..

Comments……………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………………
.........................................................................................................................
……………………………………………………………………………………….…..

Signature/stamp……………………………………………..date……………………..



**Fomu Namba……….**

**ASSURAN ES SALAAMTEL. 0767006553/0742500221**
**WEBSITE: Zawadischools.ac.tz CE SECONDARY SCHOOL**

**P.O BOX 91843 DAR ES SALAAM**

PASSPORT SIZE

YA

MWANAFUNZI

**FOMU YA USAJILI (Ijazwenakurudishwashuleni)**

**SEHEMU A:**( Ijazwenamwanafunzimwenyewe)

JINA LA MWANAFUNZI………………………………………………………

TAREHE YA KUZALIWA…………………………….MAHALI (wilaya)……………………
URAIA……………………….DINI……………………DHEHEBU………………………..
SHULE YA MSINGI ULIYOSOMA……………………NAMBA YA MTIHANI ps….....
MAHARI UNAPOISHI KWA SASA……………………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI**
Mimi……………………….. nakubali kutumia nafasi hii adimu ya kidato cha …...
Ninakiri kuwa nimesoma na kuelewa maelezo yote ya kujiunga na shule hivyo nitazingatia kwa muda wangu wote niwapo shuleni. Nitakubali kurekebishwa na walezi endapo nitakwenda kinyume na kusoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yangu yote kwa wastani wa shule ambao ni sitini na tano [65] kwa kila somo na jumla.
Sahihi ya mwanafunzi……………………………….tahere……………………………….

Uthibitisho wa mkuu wa shule baada ya usaili kufanyika.

Jina……………………………………..sahihi na
………………………….muhuri…………..………………………tarehe………………….

Amepokelewa kwa njia ya

i/. kuhamia [ ]

Ii/.Ameanza kidato cha kwanza [ ]

Alama za mtihani wa usaili……………………………………………………………………….

Amelipia ghrama za usajili keshi ndiyo[ ] hapana [ ]



**TAARIFA ZA MZAZI.**

**SEHEMU B**: Ijazwe na mzazi au mlezi

assport
ize ya
nzazi/mlezi
a kiume

Passport
size ya
mzazi/mlezi
wa kike

1. JINA LA MZAZI AU MLEZI…………………………..KAZI……………
2. ANUANI……………………………SIMU…………………………..……..
3. MAHALI NINAPOISHI………………………………..…………………

**AHADI YA MZAZI/MLEZI KULIPA ADA NA MICHANGO MINGINE**

Mimi …………………………………mzazi/mleziwa ……………………….. wa kidato cha …………… mwaka wa ……………..katika shule ya sekondari Assurance, ninakiri kupokea, kusoma na kuelewa tararibu zote zilizopo kwenye maelekezo ya kujiunga na shule ya sekondari Assurance. Iwapo mwanangu atakiuka taratibu hizo nitakuwa tayari kukubali hatua zitakazochukuliwa dhidi yake, ili kuepusha usumbufu, thibitisha nakuahidi kuwa tayari kulipa ada na michango yote kwa wakati kama ilivyoainishwa katika hati ya malipo kwa ajili ya maendeleo ya shule na mwanafunzi

Jina na Saini ya Mzazi/Mlezi wa kiume…………………….…tarehe…………….simu………

Jina na Saini ya Mzazi/Mlezi wa kike………………………tarehe…………….simu……….